



# ***Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo***

## **MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 AGOSTI, 2022 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11- 20 AGOSTI, 2022.**

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 AGOSTI, 2022.**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii iliendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu na kupelekea mchango katika kusukuma hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuimarisha mwendokasi wa upepo. Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani, hali ambayo ilileta mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi yetu. Katika upande wa kati mwa bahari ya Pasifiki, joto lilikuwa chini ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango katika kuchochea visababishi vya mvua katika nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango mkubwa katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA**

Kwa ujumla, maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu na yenye hali ya ubaridi. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi vikiambatana na vipindi vifupi vya upepo mkali viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi.

### **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 AGOSTI, 2022**

#### **2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 AGOSTI, 2022**

Kipindi hiki kinatarajiwa kuendelea kutawaliwa na kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) pamoja na kudhoofu kwa migandamizo mikubwa iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia). Hali hii itaendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu na hivyo kuwa na mchango katika

*Kwa Mawasiliano:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd  
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

kusukuma hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani na eneo la kati mwa bahari ya Pasifiki, joto la bahari linatarajiwa kuendelea kua la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kutokuwa na mchango mkubwa katika kuchochea visababishi vya mvua katika maeneo mengi ya nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango mkubwa katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 AGOSTI, 2022**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vichache vya ngurumo za radi vinatarajiwa.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu yakiambatana na hali ya ubaridi pamoja na vipindi vifupi vya mvua nyepesi..

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Kwa Mawasiliano:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd  
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8  
Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)